

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 29 Januari, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Mjumbe afuataye aliapa Kiapo cha Uaminifu na kukaa katika nafasi yake Bungeni:-

Mhe. Getrude Pangalile Rwakatare

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, tarehe 16 Desemba, 2007, tulipotelewa na mwenzetu Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mbunge wa Kiteto. Kama ilivyo kawaida, kabla hatujaendelea mbele, nawaomba tusimame wote kwa dakika moja ili tuweze kumkumbuka. Ahsanteni sana.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walisimama kwa Dakika Moja Kumkumbuka Mheshimiwa Benedict Losurutia)

T A A R I F A Y A S P I K A

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninayo heshima kutoa taarifa kama ifuatavyo:-
Kwanza, ni kuhusu Miswada ya Sheria iliyopata kibali cha Mheshimiwa Rais. Waheshimiwa Wabunge, itakumbukwa kwamba Bunge katika Mkutano wake wa Tisa pamoja na shughuli nyingine ilipitisha Miswada tisa ya Sheria ya Serikali. Miswada hiyo yote tisa ilipata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni Sheria za nchi. *(Makofi)*

Muswada wa kwanza ni “*The Public Service (Amendment) Act, 2007* ambao unakuwa ni Sheria Na. 18. Pili, *The Written Laws (Miscellaneous) Act Na.2* wa Mwaka

2007. Tatu, *The Environmental Act Practitioners Registration Act Na. 20* wa Mwaka 2007. Nne, *The Medical Radiology and Imaging Professional Act Na. 21* wa mwaka 2007. Tano, *The Health Practitioners Act Na. 22* wa mwaka 2007. Sita, *The Procurement and Supplies Professional and Technicians Board Act Na. 23* wa mwaka 2007. Saba, *The Engineers Registration Board (Amendment) Act Na. 24* wa mwaka 2007. Nane, *The National Construction Council (Amendment) Act Na.25* wa mwaka 2007. Tisa, *The National Bank of Commerce Reorganization and Vesting of Assets Liabilities Na. 2* ambao unakuwa Na. 26 wa mwaka 2007. Hii ina maana kwamba kwa mwaka wa 2007 Bunge letu hili limetunga jumla ya Sheria 26. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia katika kipindi cha maswali, kama mlivyoona tumetumia dakika 10 kwa mambo mbalimbali yasiyohusiana na maswali. Sasa ili tuwatendee haki wanaouliza maswali, natoa taarifa ya awali kwamba nitaongeza dakika 10 hapo mwisho ili tuweze kukamilisha maswali yote.

Pili, naomba kumkaribisha sana Bungeni Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare, aliyeapishwa hivi punde. Karibu sana na tunakutakia utumishi mwema katika Bunge letu. (*Makofi*)

Na. 1

Baraza la Mawaziri Kuelezea Bajeti Mikoani

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikuwa na nafasi ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa Bajeti ndani ya kipindi cha Bunge la Bajeti kwa utaratibu wa kila Wizara kuelezea bajeti yake:-

(a)Je, ni sababu zipi zilizosababisha Mawaziri kutawanywa Mikoani kuelezea utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2007/2008?

(b)Je, kiasi gani cha fedha kilitumika katika ziara hizo kuwalipa Mawaziri, Wasaidizi wao na Watendaji waliohusika?

(c)Je, kwa nini Serikali isingetekeleza yaliyoahidiwa na kila Wizara ili wananchi wajionee mafanikio ya bajeti badala ya kuwatuma Mawaziri kwenda Mikoani kuielezea Bajeti?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 6.065 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa shughuli zake na maendeleo ya wananchi. Kati ya fedha hizo, Serikali imepanga kutumia shilingi trilioni 3.141 ambazo ni sawa na asilimia 52.1 ya Bajeti yote kwa ajili ya sekta tano (5) za vipaumbele ambazo ni Elimu, Miundombinu, Afya, Kilimo na Maji. Aidha, katika kutekeleza sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi yaani (*D by D*), Serikali imehamisha kutoka Serikali Kuu kiasi cha shilingi bilioni 286 kwenda kwenye Halmashauri. Kiasi hiki ni kikubwa kupelekwa kwenye Halmashauri kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuwatuma Mawaziri wake Mikoani ili kuhimiza Halmashauri na Waheshimiwa Madiwani kuimarisha usimamizi wa fedha za Serikali zilizotengwa katika maeneo yao ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa na Serikali katika Bajeti ya mwaka 2007/2008. Aidha, kupitia mikutano ya hadhara, wananchi walihimizwa nao wachangie nguvu zao ili fedha zilizotengwa zilete manufaa makubwa zaidi.

Pili, wananchi wasaidiane na Serikali kusimamia fedha zilizotengwa na wakiona utekelezaji hafifu watake maelezo kuhusu matumizi ya fedha hizo. Serikali imewataka wananchi watambue kuwa fedha za Bajeti ni kodi zao, hivyo wasimamie matumizi yake ili zitumike vizuri kwa kazi zilizokusudiwa.

(b) Kila Wizara ilitumia fedha zilizoko katika Bajeti ya kawaida na ilijumuishwa katika safari za kawaida za Mawaziri na wasaidizi wao ikiwa ni sehemu ya kazi zao za

kila siku za majukumu yaliyo chini ya Wizara zao. Jumla ya fedha zilizotumika ni shilingi 142,960,000.

(c) Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, Serikali iliona kuwa ili kuleta manufaa kwa fedha nyingi zilizotengwa hasa katika sekta za vipaumbele, ni vyema kutoa maelezo ya ufafanuzi kwa viongozi wa Halmashauri na wananchi ili kila kilichoahidiwa na Wizara husika kiweze kutekelezwa. Aidha, ziara hizi zilitoa fursa kwa wananchi kueleza kero zao kwa Mawaziri na kisha kupatiwa majibu sahihi. Hatua hii iliwatia moyo sana wananchi na waliahidi kushirikiana na viongozi wao wa Halmashauri ili kuhakikisha wanapata mafanikio katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza moja la nyongeza.

Kwa kuwa kote walikokwenda Mawaziri kuna Wabunge na Wabunge kazi yao ni kuwakilisha wananchi, kupeleka maelezo ya Serikali au majibu ya hoja zao, sasa Mawaziri wakifanya kazi hiyo Wabunge wafanye kazi gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ni vizuri tukatambua kwamba Wabunge wana wajibu mkubwa katika Majimbo yao lakini ni vizuri pia wananchi wakaelewa kwamba pamoja na wajibu mkubwa walionao Wabunge lakini wana rasilimali chache sana za kuwawezesha kutekeleza wajibu huo kwa ufanisi unaokusudiwa. Ndiyo maana katika Bunge hili tunajitahidi na tulitaka tuhakikishe kwamba tunaweza kuwapatia fursa ya kuweza kuwafanya mkazunguka. Sasa Mawaziri walivyokwenda kule ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba yale ambayo wanayapanga yanatekelezwa kwa ufanisi uliokusudiwa. Wabunge kazi yao kwenda kule ni kufuatilia kuhakikisha kwamba ule utendaji na ahadi zile kweli zinatekelezwa.

Kwa hivyo uhusiano wa Wabunge na Serikali ni uhusiano wa ushirikiano yaani ku-*compliment initiative* za Serikali. Kwa hivyo, hata siku moja hatutaweza kusema kwamba Serikali itakaa chini kutokufanya ziara eti kwa sababu kuna Wabunge katika Majimbo. Wabunge wataendelea kufanya kazi na Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inawapatia Wabunge rasilimali mbalimbali za kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao katika Majimbo yao lakini Serikali itafuata wananchi wale ambao waliwapa kura na kuhakikisha kwamba yale ambayo waliwaahidi wanatekeleza kadri ilivyokusudiwa. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi ya Mheshimiwa Waziri ambapo amejibu vizuri sana na amekiri kabisa kwamba Wabunge hawana nyenzo za kutosha, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuhakikisha kwamba Wabunge wanapatiwa nyenzo hizo ili waweze kufanya kazi zao kwa sababu wako karibu sana na wananchi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN): Mheshimiwa Spika, napenda wananchi watambue kwamba pamoja na nia njema ya Serikali kuongeza nyenzo kwa ajili ya Wabunge ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi lakini hawatafanya kazi kwa niaba ya Mawaziri. Mawaziri wataendelea kupita kwenye Majimbo na kuzunguka nchi nzima kuangalia kero.

Baada ya kusema hivyo, Serikali na nyote mnajua tulishatayarisha Rasimu ya Muswada kwa ajili ya kuweza kuwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Bado tunaendelea na jitihada hizo na tushirikiane kwa pamoja ili basi hatimaye tuweze kufanikiwa katika kuanzisha Mfuko wa Wabunge wa Maendeleo wa Jimbo ili Wabunge waweze kupata rasilimali ya kuwasaidia kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Waziri.

Ameeleza kwamba wananchi walifurahishwa sana kwa Mawaziri wetu wa Mawazara kutembelea sehemu mbalimbali. Je, Serikali iko tayari kufanya ziara hizi za Mawaziri ili wananchi wetu waweza kuyajua mambo ya ndani kabisa ya Mawazara?

SPIKA: Mheshimiwa, naomba urudie swali lako naona halikukaa vizuri, hebu lilenge ili litoe fursa kwa Mheshimiwa Waziri kujibu.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Kwa kuwa wananchi wamefurahishwa sana na ziara hizi za Mawaziri, je, Serikali itakuwa tayari pale wanapopata nafasi kwa Mawaziri hawa kutembelea na kueleza mambo ya ndani ya Wizara zetu na vile vile wafike Zanzibar kwa ziara hizi? *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Nilikuwa nina hakika kwamba swali lilikuwa halijakamilika. Sasa majibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN): Mheshimiwa Spika, kwanza ni vizuri tukakubali kwamba katika awamu hii tumekuwa na Waziri anayeshughulika na masuala ya Muungano. Lakini masuala ya Serikali ambayo yanaingia katika zile sekta ambazo ni za Kimuungano, Mawaziri wana mawasiliano na huwa wanafanya kazi na kutembelea katika maeneo hayo. Sote ni mashahidi mfano Wizara ya Sayansi na Elimu ya Juu, Waziri, Mawaziri wanakwenda kule na wanafanya ziara na wanajua yanayofanyika.

Lakini kwa sababu nchi yetu ni nchi ambayo tuna Muungano Zanzibar na Tanzania Bara, tutaendeleza mahusiano hayo kupitia mikutano mbalimbali ya hadhara, kupitia viongozi kutembeleana ili wananchi wajue zaidi yote yanayoendelea katika Wizara mbalimbali. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe kwamba tutamtumia zaidi Waziri wetu wa Muungano katika kufikisha ujumbe na kufanya wananchi wakaelewa yale ambayo yanafanyika katika Serikali hii na Serikali ya SMZ.

Barabara Jimboni Kisesa

MHE. LUHAGA J. MPINA aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara za Vijiji na Kata Jimboni Kisesa, Wilayani Meatu ni mbovu sana na hazipitiki kabisa na kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii kuwa ngumu kama vile usafirishaji wa Pamba, Mahindi, Mtama, Mifugo na bidhaa zingine na kwa upande mwingine akinamama wajawazito, watoto na wagonjwa wengine kufa bila matibabu na Sekondari za Kata kukosa mawasiliano na kwa kuwa, fedha zinazotengwa na Serikali kupitia Halmashauri za Miji/Wilaya (*Road Fund*) hazitoshi kabisa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kutenga fedha za kugharamia barabara ya kutoka Malwilo-Lingeka-Mwabulutago-Mwamhongo hadi Mwasengela na ile ya kutoka Lubiga-Mwandu Itinje hadi Mwabusahi?

(b) Je, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa darala la Mto Lubiga?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Malwilo-Lingeka-Mwashata (Km 17.5) ni barabara ya Wilaya (*District Road*) na barabara ya Lingeka-Mwabulutago-Mwamhongo-Mwasengela (Km. 9.5) ni barabara ya ujazio (*Feeder Road*). Barabara ya Lubiga – Mwandu – Itinje – Mwabusalu (18.5) ni barabara ya Wilaya. Barabara zote hizi ziko katika kiwango cha udongo. Kutokana na umuhimu wa maeneo hayo, barabara hizo zinapopita Halmashauri ya Wilaya ya Meatu katika mwaka wa fedha 2007/2008 imetenga jumla ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga barabara ya Lingeka-Mwabulutago-Mwamkongo-Mwasengela kwa kiwango cha changarawe. Fedha hizo zitataka kwenye Mradi wa *District Agricultural Sector Programme* (DASIP).

Aidha, Sh.11,276,920 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida (*routine maintenance*) ya barabara ya Lubiga-Mwandu Itinje-Mwandusala. Kutokana na umuhimu wa barabara hii kwa kuunganisha Wilaya ya Meatu na Bariadi, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imeomba barabara hii ipandishwe hadhi kuwa barabara ya Mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, Mto Lubiga upo katika barabara ya Nguhoboko-Mwandoya-Kisesa (Km 70) ambayo ni barabara ya Wilaya ikiwa katika kiwango cha changarawe na inaunganisha Wilaya ya Meatu na Bariadi. Kutokana na fedha kidogo

zinazopatikana, Halmashauri iliamua kujenga *Drift* 29 katika barabara hiyo ikiwa ni pamoja na katika Mto Lubiga.

Serikali inaatambua umuhimu wa daraja la Mto Lubiga. Kwa kutambua umuhimu huo, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imejenga *Drift* linalosaidia kuvuka mto huo wakati wa mvua za masika na kiangazi. Lakini kwa kuwa wakati wa mvua kubwa maji hupita juu ya *Drift* hasa wakati wa masika inakuwa vigumu kuvuka mto, hivyo kuwalazimu watumiaji wa *Drift* hilo kusubiri hadi maji yapungue. Kutokana na umuhimu wa daraja kuwapo, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imepeleka mapendekezo katika Bodi ya Barabara ya Mkoa kuomba barabara ya Ng'hoboko – Mwandoya - Kisesa yenye urefu wa Km.70 kupandishwa hadhi kuwa barabara ya Mkoa. Upandishwaji hadhi wa barabara hiyo utasaidia uimarishaji wake ikiwamo ujenzi wa madaraja katika Mto Lubiga.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana na Serikali kwa kukubali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo muhimu pamoja na daraja hilo muhimu. Ninalo swali moja dogo moja la nyongeza.

Katika Bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali ilitenga fedha kujenga barabara ya kutoka Mwakasumbi kwenda Mwashata. Barabara hiyo imejengwa lakini bado kuna kilomita 2 hazijajengwa. Kwa kuwa kilomita 2 hizo zilizobaki ni korofi sana na bado kuna kijito ambacho kinawafanya wananchi wapate adha kubwa na kero kubwa na kwa kuwa hata mimi nilipokuwa kwenye ziara, gari langu lilitumbukia mle na wananchi wakaja kunisaidia kulitoa lakini wakaniambia kuwa adha hii wamekuwa wakiipata miaka nenda rudi...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ulenge swali la nyongeza sio maelezo.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Je, Serikali sasa kwa kutambua umuhimu huo mkubwa, imejipanga vipi kumalizia hizo kilomita 2 zilizobaki ambazo wananchi wanapata adha kubwa na kunipunguzia msugurano mimi na wananchi wangu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya barabara hii ya Mwakasumbi hadi Mwashita na kweli zilibaki kilomita 2 ambazo ni sehemu korofi. Kwa kutambua umuhimu wa sehemu hiyo hiyo korofi, Serikali kwa mwaka huu 2007/2008 imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 20 kwa ajili ya utengenezaji wa sehemu hiyo korofi.

Na. 3

Wabunge Kusimamia Matumizi ya Fedha za Halmashauri

MHE. STEPHEN J. GALINOMA aliuliza:-

Kwa kuwa, Waziri Mkuu katika hotuba yake ya kufunga Mkutano wa Bajeti, 2007, aliagiza na kusisitiza umuhimu wa Wabunge kusimamia matumizi ya fedha katika Halmashauri za Mitaa lakini uzoefu unaonyesha kuwa, utaratibu uliopo haumpi Mbunge Madaraka/Mamlaka ya kudhibiti Serikali za Mitaa pale ambapo panatokea utovu wa nidhamu katika matumizi hasa ikitiliwa maanani kuwa, Mbunge kama Diwani hana uwezo zaidi ya Madiwani ambao wengine hutegemea hisani zaidi na imekuwa ni kawaida kwa Halmashauri nyingi kuwakwepa Wabunge wakati wa kupanga vikao vyao hasa vya fedha:-

Je, isingekuwa jambo la maana kutoa mwongozo utakaoondoa uwezekano wa utatanishi katika utekelezaji wa maelekezo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Hotuba ya kuhitimisha Mkutano wa Nane wa Bunge la Bajeti Mwaka 2007/2008, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitukumbusha sisi Wabunge kuhusu jukumu na ushiriki wetu tukiwa viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na pia Wajumbe wa Baraza la Madiwani la Halmashauri zetu na baadhi yetu wengi wetu tukiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu inayohusika na masuala ya Fedha, Mipango na Uongozi.

Hivyo, tunawajibika kisheria kushirikiana na Madiwani kusimamia matumizi ya fedha za Halmashauri na shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa unaongozwa na kutekelezwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali iliyowekwa na Mamlaka zilizoundwa kisheria ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Viongozi wa Halmashauri kwa maana ya Waheshimiwa Madiwani na Wabunge ndiyo wanaohusika katika kufanya uamuzi unaohusu shughuli za Halmashauri na uamuzi huo unafanyika kupitia kwenye vikao mbalimbali vya Kamati na Mabaraza ya Madiwani katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinao utaratibu wa kuandaa na kuidhinisha ratiba ya mwaka ya vikao vya Kamati zote na Mabaraza ya Madiwani. Mkutano wa kawaida wa mwaka unaofanyika kila mwezi Desemba ndiyo unaojadili agenda ya kupitisha ratiba hiyo ya vikao vya Kamati na vikao vya Mabaraza ya Halmashauri. Inapojitokeza kuwepo umuhimu wa kufanya marekebisho ya ratiba, Mkurugenzi wa Halmashauri huwafahamisha rasmi wajumbe ikiwa ni pamoja na sababu za mabadiliko ya ratiba. Kwa kuzingatia madaraka na kazi za Halmashauri, uendeshaji wa vikao hivyo hufanyika kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu zinazotungwa na Halmashauri zenyewe na kuidhinishwa na Waziri mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni mzuri kwani unamshirikisha mjumbe yaani Diwani pamoja na Mbunge:-

(a) Kushiriki kwenye vikao kwa tarehe, mahali na muda utakaoamuliwa na Halmashauri.

(b) Kutoa taarifa ya maandishi kuelezea mawazo yake kwa agenda ya kikao au kuwasilisha agenda anazotaka zijadiliwe kwenye Kamati au Baraza la Madiwani na kutolewa uamuzi.

Kwa maana hiyo, hakuna sababu ya msingi ya kuwepo kwa mwongozo wa jumla kwa Halmashauri zote nchini kuhusu ushiriki wa Wabunge kwenye kusimamia matumizi ya fedha za Halmashauri. Kwa sasa, Sheria za Serikali za Mitaa, Kanuni za Kudumu za Halmashauri na Miongozi iliyopo inakidhi matumizi ya fedha za Halmashauri ambayo inazingatia bajeti zinazoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha tunawajibika kuhudhuria vikao vya Halmashauri. Pale ambapo tunashindwa kufanya hivyo, basi ni wajibu wetu kutoa taarifa rasmi ya kuchangia kwa maandishi mawazo yetu kwenye agenda za vikao. Kwa kuwa kila Halmashauri inazo Kanuni zake za Kudumu za uendeshaji shughuli za Halmashauri, namshauri Mheshimiwa Galinoma azipitie upya Kanuni hizo na pale anapoona kuna ulazima wa kuziboresha, awasilishe hoja kwenye vikao vya Halmashauri ili ziweze kujadiliwa na kutolewa uamuzi kadri itakavyoonekana inafaa.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mabaraza ya Halmashauri zetu hukutana mara nne tu kwa mwaka na kwa kuwa kanuni za fedha zilizopo huwaongoza tu wale wanaoweka mahesabu, je, kuna Miongozo gani iliyowahi kutolewa kuwapa ufahamu Madiwani katika jukumu hili la kusimamia matumizi ya fedha?

(b) Licha ya ukaguzi unaofanywa mara kwa mara na CAG, je, Serikali yenyewe ina utaratibu au mipango gani ya kusimamia matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa?

SPIKA: Kabla ya Mheshimiwa Waziri hujajibu, tutafanya mabadiliko kwa sababu naona inachukua muda wanaojibu maswali kurudi pale kwa zamani. Kwa hiyo, ningeomba sasa Waheshimiwa Mawaziri wanaojibu wakae kiti cha Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na baadaye tutamwomba pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Masuala ya Siasa, baadaye asogee ili sasa sehemu hiyo ya viti viwili ndiyo iwe ya Waheshimiwa Mawaziri kujibu maswali. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kanuni ambazo ndizo zinazoendesha shughuli za Halmashauri, kila mwezi Kamati ya fedha inakutana. Katika

ajenda muhimu ambazo zinazingatiwa na Kamati hiyo, ni hasa mapato na matumizi ya Halmashauri. Mkusanyiko wa taarifa za miezi mitatu ambazo zinachambuliwa na Kamati hiyo huwa zinawasilishwa katika Baraza la Madiwani kila miezi mitatu. Kwa hiyo, kwa kuzingatia utaratibu huo, naamini ni fursa nzuri tu kwa Waheshimiwa Madiwani katika vikao vya kila miezi mitatu wanapotizama sasa matokeo ya mjadala katika Kamati zile kuwapa fursa ya kuzingatia maeneo ambayo bado wanaona yaharidhishi.

Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, hakuna tatizo hata kidogo kama itaonekana utaratibu huu bado haukidhi mahitaji. Tuko tayari kushirikiana ili tuweze kufanya marekebisho ambayo mnaona yanaweza yakasaidia zaidi lakini kwa sasa utaratibu huo ndiyo unaotumika na kwa sehemu kubwa unatosheleza.

Kuhusu swali la pili, kwanza tunaomba kuishukuru sana ofisi ya CAG kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wanafanya kazi nzuri sana. Lakini nataka vilevile nizishukuru sana Kamati mbili za Bunge ile Kamati ya Utawala ambayo na sisi TAMISEMI tupo chini yao lakini vilevile Kamati ya LAAC ambao nao wanapata fursa ya kutembelea Halmashauri mbalimbali na kujiridhisha na utendaji na hasa usimamizi wa fedha. Vyombo hivi ni muhimu sana katika kuendelea kusimamia fedha za umma. Lakini kwa upande wa Serikali, ina utaratibu madhubuti sana kwenye eneo hili.

Moja, tumehakikisha kwamba tunakuwa na Kamati za *Audit* katika kila Halmashauri. Sasa hili ni agizo kutoka Serikali Kuu ambalo linatuwezesha muda wote kufahamu kinachoendelea ni nini. Kwa upande mwingine Halmashauri zote zinatakiwa kuwasilisha taarifa zao za mapato na matumizi katika kila Halmashauri kwenye Sekretarieti ya Mkoa kwa maana ya Mkuu wa Mkoa ambapo Sekretarieti yake imepewa jukumu la kusimamia kwa karibu sana matumizi ya fedha. Nao ni mfumo ambao upo na ambao umetusaidia vile vile kuweza kuona kwa karibu ni nini kinaendelea katika Halmashauri zetu.

Lakini si hiyo tu, Mawaziri wa kila Sekta nao wanafanya mizunguko katika Halmashauri zetu kuhusiana na maeneo yanayohusu sekta zao kama vile maji, mifugo kwa sababu fedha hizi zinapelekwa pale kisekta na wao wanapobaini mapungufu yoyote ni wajibu wao vilevile kuisaidia Serikali iweze kufahamu. Lakini mimi na Naibu Waziri naamini wote ni mashahidi tunajitahidi sana kuzungukia maeneo haya na kwa kuwa tunayafahamu kwa karibu, tumejitahidi sana kubaini matatizo na kuchukua hatua zinazostahili kwa wakati huo tunapopata nafasi ya kuzungukia. Yote haya ni mjumuisho wa aina mbalimbali za kusimamia Halmashauri zetu na hasa matumizi ya fedha.

Na. 4

Wafanyakazi wa Shamba la Kitulo

MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE aliuliza:-

Je, ni nini hatma ya wafanyakazi wa shamba la Kitulo ambao kwa miaka ya nyuma walikuwa chini ya Shirika la *DAFCO* na baadaye kuanzia mwaka 2004 wakaajiriwa na Serikali kwa muda?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Shamba la Kitulo lilikuwa likimilikiwa na iliyokuwa Kampuni ya Ng'ombe wa Maziwa Tanzania (*DAFCO*) kuanzia mwaka 1975 hadi mwaka 2004 lilipochukuliwa na Wizara kutokana na maamuzi ya Serikali ya mwaka 2002. Maamuzi hayo yalielekeza shamba hilo kugawanywa ili eneo kubwa la (hekta 13,500) liendelezwe kama Hifadhi chini ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) na sehemu ndogo iliyobaki (hekta 5,000) iendeleo kutumika kwa shughuli za uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo. Kutokana na maamuzi hayo, utumishi wa wafanyakazi wa shamba hilo ulihamishiwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa lililokuwa shamba la *DAFCO/Kitulo* walipatiwa ajira ya muda kutokana na kibali kilichotolewa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tarehe 01 Oktoba, 2003 kilichoidhinisha watumishi hao kuingizwa kwenye ikama ya Serikali. Kibali kilielekeza watumishi 81 wa Mashamba ya Kitulo na Ngerengere waajiriwe na waingizwe kwenye “*Payroll*” kwa kuzingatia vigezo na misingi iliyoainishwa katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Kati ya Watumishi hao 65 wa shamba la Kitulo, kwa sasa wamebaki 63 baada ya mmoja kuhamishiwa shamba la *Sao Hill* na mwingine kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu kufariki dunia.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utekelezaji unaotokana na kibali hicho ni kuwa watumishi wote 63 wa shamba la Kitulo wamepatiwa ajira ya kudumu Serikalini tangu tarehe 26 mwezi huu, mwaka huu katika nafasi zifuatazo. Maafisa Migufo wawili, Maafisa Mifugo Wasaidizi wanne, Wahudumu wa mifugo 33, Walinzi nane, Madereva saba, Mafundi Mchundo watatu, Wahasibu wawili, Maafisa Ugavi wawili na Wahudumu wa Ofisi wawili. Watumishi wote hao wanapata mishahara kwa kuzingati vyeo vyao na wameendelea kupandishwa vyeo vyao sawa na watumishi wengine wa Serikali.

MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, kwanza, kama inavyoonyesha katika majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo kwa kweli ni mazuri na ya kina kwamba kibali cha wafanyakazi hawa kuajiriwa kwa ajira za kudumu kilitolewa mwaka 2003 na imetekelezwa juzi yaani Jumamosi tarehe 26/ 01/2008, ningependa kujua ni nini kilifanya utekelezaji huo ukachelewa kiasi hicho?

Lakini pili, nini hatma ya mafao yao kwa kipindi hicho cha mwaka 2003 mpaka juzi 2008 lakini vilevile kipindi cha mwaka 1975 mpaka 2003 wakati walipokuwa *DAFCO*?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mahenge kwa kujali wananchi wote waliopo kwenye Jimbo lake la Makete. (*Makofi*)

Kuhusu kuchelewa kwa watumishi hawa kupewa ajira za kudumu, ni masuala ya utaratibu tu wa kiutumishi lakini cha msingi ni kuwa tangu walipokoma kuwa watumishi wa *DAFCO* hadi walipohamishiwa Serikalini katika maana ya kwanza kwa muda na sasa ni ajira ya kudumu ni kuwa mafao yao yote yaani malimbikizo ya mishahara, wamelipwa.

Na. 5

**Vifaa vya Kutafiti magonjwa
Yanayoambukiza Wanadamu**

MHE. SALIM HEMED KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa, *concern* kubwa ya dunia kwa sasa ni magonjwa yanayoambukiza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu (*zoonotics*) kama vile *RVF*, mafua ya ndege na kadhalika na kwa kuwa, vituo vyetu vingi vya utafiti wa magonjwa hayo havina vifaa vya kutosha vya utafiti na kinga kwa Madaktari wetu wa mifugo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, kwa hali hiyo maabara zetu sasa zinahatarisha maisha ya Madaktari wetu wa Mifugo?

(b) Je, kuna mikakati gani wa pamoja kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo katika kukabiliana na magojwa ya aina hiyo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama (*zoonotic diseases*) yanazidi kuongezeka. Kutokana na hali hii, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua za kupunguza hatari ya magonjwa haya kuambukiza Madaktari wetu wa Mifugo na jamii kwa ujumla. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kununua mavazi na vifaa maalum vya kujikinga (*personal protective equipment; PPE*) kwa ajili ya Madaktari na wataalam wengine wakati wa kufanya uchunguzi na wanapokuwa wanachukua sampuli zenye uwezekano wa kuwa na viini vya magonjwa. Wizara yangu imetoa jumla ya seti 1,500 za vifaa vya kujikinga ikiwa ni pamoja na seti 700 kwa ajili ya Madaktari na wataalam wa Wizara ya Maendeleo ya

Mifugo, seti 300 kwa ajili ya Mdaktari na wataalam wa Wizara ya Afya, seti 200 kwa ajili ya Madaktari na wataalam katika vyuo na vituo vya utafiti. Seti 300 zimebaki bohari kwa ajili ya dharura.

(ii) Kutumia vyombo maalum vyenye viwango vilivyoainishwa na Shirika la Afya Duniani (*WHO*), vya kusafirisha sampuli zenye viini vya ugonjwa.

(iii) Kuweka kabati maalum (*biosafety cabinets*) kwenye Maabara Kuu ya Mifugo ya Temeke na kwenye Vituo vya Kuchunguza Magonjwa ya Mifugo vya Kanda. Wizara imekwishanunua *biosafety cabinets* kwa ajili ya vituo vya Mwanza, Tabora, Arusha, Iringa, Mtwara na Mpwapwa. Ufungaji (*installation*) wa kabati hizo uko katika hatua za mwisho kukamilika.

(iv) Kuwa na jengo maalum lenye teknolojia ya kisasa katika Maabara Kuu ya Mifugo ya Temeke, ya kuhakikisha kuwa hakuna uwezekano wa viini vya ugonjwa kuambukizwa kwa watu au kuingia kwenye mazingira.

(b) Mheshimiwa Spika, iko mikakati mingi ambayo imeandaliwa kwa pamoja na Wizara yangu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa yanayoambukiza wanyama na binadamu. Mikakati hiyo ni pamoja na ule wa kukabiliana na ugonjwa wa mafua makali ya ndege (*National Avian Influenza Emergency Preparedness and Response Strategic Plan – 2006/08 – 2008/09*), mkakati wa kutokomeza kichaa cha mbwa (*Strategy for Rabies Control in Tanzania*) na mkakati wa kuondoa ndorobo na kudhibiti ugonjwa wa nagana kwa mifugo na malale kwa binadamu (*National Strategy for Intergranted Management of Tsetse and Trypanosomiasis in Tanzania*). Aidha Wizara hizi mbili zina Kamati za pamoja za wataalamu kwa ajili ya kutathmini na kushauri Serikali juu ya mbinu bora za kukabiliana na magonjwa yaliyotajwa.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Hivi karibuni kulikuwa na matembezi Mpwapwa na kule Arusha kuangalia utafiti katika vituo vya utafiti wa wanyama na tumejionea kulikuwa na uhaba mkubwa wa vifaa vya utafiti, uchakavu mkubwa pamoja na malipo duni sana ya wataalam wetu. Je, hali hii ikiachiwa kuendelea, halitaongeza lile wimbi la wataalamu wetu kuhama nchi yetu na kuelekea nchi jirani ambako kuna mazingira bora ya kazi na maslahi bora?

(b) Katika mikakati hii ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja, kule tulikotembelea haieleweki, wataalam hawaelewi chochote na anasema kwamba watu wa afya na watu wa mifugo wanakutana tu baada ya ugonjwa unapotokea. Je, hakuna uwezekano kwa mikakati hii kuishia ngazi ya Wizara tu na sekta ya utendaji ikawa haielewi na yanapokuja matatizo ya ugonjwa hali ikawa ni ngumu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, mikakati yote niliyoieleza katika jibu la msingi kwa vyovyote vile imeshirikisha wataalam wote wa Wizara yangu na wale wa Afya ili kusudi utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mikakati hiyo uweze kufanyika kwa makini. Kwa hiyo, napenda kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuwa watumishi hawa wanafahamu kazi zote wanazopaswa kuzifanya kwa kuwa wanashirikishwa katika uandaaji wa mipango hii niliyoisema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi pamoja na maslahi duni aliyosema Mheshimiwa Mbunge, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Hemed kuwa Serikali imekuwa ikichukua hatua za makusudi za kuboresha maslahi na vitendea kazi kama nivyoieleza kwenye majibu yangu ya msingi kama vile ununuzi wa makabati na ukamilishwaji wa maabara ya kisasa kabisa pale Temeke na kuboresha Vituo vya Uchunguzi wa magonjwa vilivyoko Mikoani ili kuhakikisha kuwa wataalamu wetu wanafanya zile kazi katika mazingira ambayo ni salama na wanatimiza wajibu wao ipasavyo. Kuhusu suala la maslahi, Serikali huwa inachukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha watumishi wote wa Serikali wanapata maslahi yanayowawezesha kuitumikia nchi yao vizuri.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ugonjwa unaoletwa na wanyama na kuwaambukiza mifugo, ni *foot and mouth disease*. Je, Serikali ipo tayari kutafuta dawa ya kinga kwa vile ipo na kuchanja mifugo ili ugonjwa huu upungue?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, imejipanga kukabiliana na magonjwa yote muhimu yanayoathiri mifugo ikiwemo ugonjwa wa midomo na miguu kwa Kiingereza ni *foot and mouth disease* na katika mwaka wa fedha kuna bajeti ya kukabiliana na magonjwa hayo muhimu niliyoyataja ukiwemo ugonjwa huu.

Na. 6

Tanzania Kukiuka Masharti ya Mkataba wa Kimataifa.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 11 Septemba 1976, Tanzania iliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966 (*International Covenant on Economics, Social and Cultural Rights*) na kwa kuwa tarehe 10 Septemba, 1979 Tanzania iliwasilisha ripoti yake ya kwanza ya utekelezaji wa masharti ya Mkataba huo kwa Kamati husika ya Umoja wa Mataifa:-

Je, ni nini kimesababisha Serikali yetu ya Tanzania kukiuka masharti ya Mkataba wa Kimataifa tulioridhia sisi wenyewe kwa kushindwa kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa Mkataba huo kwa kipindi cha miaka mitano kwa takribani miaka 28 mfululizo hadi leo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. CYRIL A. CHAMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania iliwasilisha taarifa juu ya utekelezaji wa masharti ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966 kwa mara ya mwisho mwaka 1979, kwa mujibu wa Ibara ya 16 ya Mkataba huo. Kuchelewa kuwasilisha kwa taarifa kwa miaka iliyofuata kunatokana na sababu za uwezo mdogo wa kiuchumi na za kiutawala ambapo mwaka 1990 jukumu la uandaaji wa taarifa hizi lilihamishwa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwenda Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Kwa sasa jukumu la kuandika ripoti lilihamia Idara ya Katiba na Haki za Binadamu, Chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali imeshaanza kuandaa rasimu ya ripoti hii, itakayojumuisha kipindi cha kuanzia mwaka 1990 mpaka sasa kwa mujibu wa taratibu za *ECOSOC (Economic and Social Council)*, ambacho ndicho chombo kinachosimamia utekelezaji wa Mkataba huu. Rasimu hii itasambazwa kwa wadau kabla ya kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Suala la kukamilika kwa ripoti hii limepewa kipaumbele kwa mwaka huu wa 2008.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kwa uelewa wake mpana wa masuala la Mikataba ya Kimataifa na nia yake nzuri ya kuikumbusha Serikali yetu kutekeleza yale tuliyoridhia.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuchelewa kuwasilisha taarifa au ripoti za miaka mitano mitano kwa miaka 28 ni kipindi kirefu mno hasa kwa nchi iliyojijengea heshima kubwa kimataifa katika masuala ya kimataifa kama Tanzania, je, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ambayo inaisimamia sasa hiyo Idara ya Katiba na Haki za Binadamu chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inalihakikishiaje Bunge hili kuwa udhaifu uliojitokeza kwa miaka 28 mfululizo hautokei tena na Watanzania tunapolilia vikao vya *ECOSOC* hatuongeti kwa kigugumizi tena?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa aliyoyatoa hapa katika Bunge lako Tukufu. Vilevile nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Mwakyembe kwa kuona kwamba masuala ya Wizara ya Katiba na Sheria ni mtambuka na kazi kubwa ni kuona kwamba Serikali yetu inawajibiki ipasavyo na kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba Wizara itawajibika zaidi na sisi tutakuwa tunafuatilia kwa karibu sana kwamba wajibu wetu wa Kimataifa unaendelea kutekelezwa ili kujijengea heshima zaidi kama yeye alivyosema.

Na. 7

Mapato Yanayotokana na Visa

MHE JOHN M. CHEYO (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)
aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania hivi sasa inapokea wageni wengi na hivyo kupata mapato kutokana na utoaji wa vibali (*Visa*) kwa wageni hao kuingia nchini:-

(a) Je, mapato ya *Visa* yanaingizwa katika mfuko gani na ni nani anayeidhinisha matumizi yake?

(b) Je, *Visa* zinazotolewa Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam zinabandikwa *sticker*?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mapato yatokanayo na utoaji wa vibali (*visa*) kwa wageni waingiao nchini hupokelewa katika akaunti za maduhuli zilizopo katika kila Ubalozi. Fedha hizo huhamishwa kwa matumizi ya kawaida ya Ubalozi kwa kibali maalum kutoka kwa Afisa Masuhuli ili mradi bajeti iliyoidhinishwa haikiukwi. Huu ni utaratibu chini ya *Retention Scheme* uliowekwa kati ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Hazina ambapo kiasi sawa hupunguzwa toka stahili ya mgao wa fedha wa Wizara kwa mwaka husika. Narudia kusema kwamba, Ubalozi hauwezi kutumia fedha hizo bila ya kupata kwanza kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambaye ndiye Afisa Masuhuli.

(b) *Visa* zote hutolewa kwa *sticker* tofuati pekee ni kwamba kuna *sticker* zinazoandikwa kupitia mashine (*Electronic Visa Stickers*) na zile zinazoandikwa kwa mkono (*manual*). *Sticker* za kuandika kwa mkono bado zinaendelea kutumika kwa baadhi ya maeneo kutokana na ukweli kwamba mashine tulizonazo hazitoshelezi mahitaji kwa nchi nzima. Kwa upande wa Uwanja wa Ndege wa Mwalim Nyerere Dar es Salaam, *Visa* zitolewazo zinatumia *sticker* ya mashine.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Swali la kwanza, kwa kuwa kumekuwa na ubadhilifu wa fedha zaidi katika baadhi ya Balozi za Heshima (*Honorary Consulates*). Je, Serikali inachukua au imechukua hatua gani kuhakikisha fedha za Serikali haziangaliwi na mtu ambaye si mtumishi wa Serikali? Ninasema hivyo kwa sababu *Honorary Consulate* si mtumishi wa Serikali. Je, Serikali

imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba fedha hizo zinaangaliwa na watumishi wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa *Visa* ni njia mojawapo ya uhusiano kati ya nchi na nchi na siku hizi wageni wetu wanaweza kupata *Visa* Dar es salaam, lakini kuna nchi nyingi ambazo ni tabu sana kwa Watanzania kupata *Visa* ya kwenda kule. Je, isingekuwa vizuri Serikali ikaambatanisha urahisi wa kupata *Visa* Dar es salaam na urahisi pia wa kupata *Visa* kwa nchi mbalimbali ambazo tunahusiana nazo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI): Mheshimiwa Spika, ni kweli Balози wa Heshima siyo Mtumishi wa Serikali lakini ameteuliwa kwa kupitia michakato ya Serikali na Mabalози wa Heshima hufanya kazi chini ya Mabalози waliomo katika maeneo yao. Ni kweli kumekuwepo na huo ubadhilifu lakini hivi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na Balози zile ambazo zinahusika na hawa Mabalози wa Heshima, ubadhilifu huo umedhibitiwa na sasa tuna utaratibu wa kuwabadilisha baadhi ya Mabalози wa Heshima ambao tumewaona siyo waaminifu. Kutokana na hali yoyote ile hatuwezi kuepuka kuwatumia Mabalози wa Heshima kwa sababu ya kutoweza kuweka Balози zetu kila mahali. Lakini, tunalihakikishia Bunge hili kwamba tutawadhibiti Mabalози hawa wa Heshima ili wawe waaminifu na waweze kufanya kazi zao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli suala la *Visa* ni suala la mahusiano kati ya nchi na nchi. Ni kweli wakati mwingine wageni wetu hupata *Visa* Dar es Salaam wakati wakiingia lakini inavyotakiwa hasa wageni wote wanatakiwa wapate *Visa* kule wanakotoka ili wajulikane hasa ni wageni wa aina gani kwa sababu kule wanakotoka ndiko wanawajua hawa watu kuliko kupata *Visa* wakiingia nchini. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, suala la *Visa* ni suala la uhusiano, kwa hiyo huwa tunawapa *Visa* kwa ajili ya kuingia nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la Watanzania kupata *Visa* katika *Airport* wanazolingia nchi za nje, hili ni suala la utaratibu wa nchi zile zinazohusika ambazo kwa kweli hatuwezi kuingilia. Ahsante!

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, ni nchi nyingi duaniani ambazo hazitoi *Visa* ya papo kwa papo na Watanzania mara nyingi hawapewi *Visa* ya papo kwa papo pale wanaposafiri, je, ni masharti yapi hasa yanayofanya baadhi ya wageni wanaoingia Tanzania wapewe *Visa* ya papo kwa papo wanapoingia mipakani lakini wengine wakataliwe *Visa* ya papo kwa papo wanapoingia mpakani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI): Mheshimiwa Spika, kweli kama nilivyosema katika jibu langu lililopita, *Visa* lazima zitolewe mtu anakotoka (*point of origin*) kwa sababu kule ndio wanaomtambua huyu mtu anayekuja nchini kwetu

Tanzania. Lakini baada ya kumchunguza na kumwona hana matatizo hasa kutokana na nchi anayotoka, ndiyo tunampa *Visa* ya papo kwa papo ili aingie nchini. Baadhi ya wageni tunawazuia kutokana na nchi wanayotoka kwa sababu kuna baadhi ya nchi ambazo zimo katika utaratibu wa *Referred Visa*. Watu hawa lazima kwanza wanakotoka waombe *Visa*, wajibiwe, ndiyo wapewe *Visa* na kuingia hapa nchini. Sasa, kama kuna wageni wamo katika nchi hizo, hawa ndiyo wakifika *airport* au mipakani, lazima wanazuiliwa kupewa *Visa* mpaka wamechunguzwa kwanza.

Na. 8

**Kupunguza Idadi ya Wagonjwa
Wanaotibiwa Nje ya Nchi.**

MHE. SUSAN A. LYIMO aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina madeni ya matibabu nchini India na Serikali inaendelea kupeleka wagonjwa huko:-

(a) Je, ni kweli kuwa Serikali inashindwa kuwatibu baadhi ya wagonjwa hapa nchini?

(b) Je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kupunguza idadi ya wagonjwa kwenda nje hasa ikizingatiwa kuwa idadi ya Madaktari Bingwa inaongezeka?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine, Wizara yangu ina wajibu wa kusimamia na kulinda afya za Watanzania. Ni nia ya Serikali kuwa wagonjwa wote watibiwe hapa nchini ili kupunguza gharama kubwa inayotokana na matibabu nje ya nchi ikiwa ni pamoja na usumbufu wanaopata wagonjwa na jamaa zao. Hata hivyo, kwa wagonjwa ambayo hatuna wataalam wake au yanahitaji vifaa tiba ambavyo Serikali bado haijavimudu, wagonjwa husika hupewa rufaa ya kwenda kutibiwa nje ya nchi hususan India ambako wanaweza kupatiwa huduma ya tiba kwa usahihi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, takriban asilimia 75 ya wagonjwa wanaopelekwa kutibiwa nje ya nchi ni watoto na wengi wao wanakuwa na matatizo ya moyo wanayozaliwa nayo (*congenital heart diseases*). Kwa kulitambua hilo, kama ambavyo nimekuwa nikiliarifu Bunge lako Tukufu, Wizara yangu ina mpango wa kuanzisha huduma ya upasuaji wa moyo hapa nchini. Mpaka sasa jumla ya wataalam 27 wamekwishapata mafunzo ya muda mrefu katika fani ya upasuaji wa moyo nchini India na Israel na tayari wamerejea nchini. Aidha, vifaa tiba kwa ajili ya upasuaji wa moyo tayari vimewasili Bandari ya Dar es Salaam na viko katika hatua ya kutolewa bandarini. Vifaa hivyo vinatarajiwa kufungwa

MOI kati ya Februari na Juni mwaka huu. Huduma ya upasuaji wa moyo inatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika ufugaji wa vifaa hivyo. Ni matumaini yetu kuwa utekelezaji wa mpango huu utasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza idadi ya wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango niliyoitaja hapo juu. Serikali inaendelea kuongeza idadi ya udhahili wa Madaktari katika kozi za Udaktari Bingwa wa fani mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kuendelea kununua vifaa tiba vya kisasa ili kuimarisha utoaji wa huduma za tiba nchini. Aidha, Wizara ina mpango wa kuziwezesha hospitali zote za Mikoa kuwa Hospitali za Rufaa. Tayari pesa zimetengwa katika bajeti kwa ajili ya ukarabati wa hospitali 11 kwa mwaka huu na zoezi linalofuata ni kusomesha wataalam na kuzipatia vifaa. Mtazamo wa Wizara ni kwamba wakati zoezi hili linaendelea Hospitali nne za Rufaa zilizopo hivi sasa zitakuwa hospitali maalum.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba asilimia 75 ya watoto wanaopelekwa nje ni wale wenye matatizo ya moyo (*Congenital Heart Diseases*) na kwa kuwa Taasisi ya Moyo (*Tanzania Heart Institute*) inafanya upasuaji wa moyo, je, Serikali inaitumiaje Taasisi ile?

(b) Kwa kuwa bado wataalamu wetu wengi wanakwenda nje kwa kile kinachoitwa *green pastures* na kwa kuwa Serikali hii imewagharamia sana Madaktari hao, je, Serikali au Wizara ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba ina-retain mabingwa hao ili waweze kufanya kazi hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Taasisi ya *MOI* ipo na inafanya operesheni. Serikali sasa hivi imekuwa ikifanya mahusiano na Taasisi hii ili kuweza kuona kwamba wagonjwa wengine wanafanyiwa operesheni pale na hivi sasa tunafanya mpango kabambe wa kuweza kuitembelea hospitali ile ili tuweze kuona ni jinsi gani tutaweza kuisaidia ili wale wagonjwa wengine badala ya kwenda nje waweze kufanyiwa operesheni pale Taasisi ya *MOI*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Madaktari wanaokwenda nje kutafuta *green pastures*, kama nilivyokuwa nikiliarifu Bunge lako Tukufu, Serikali imekuwa ikifanya mipango mbalimbali si kwa Madaktari tu lakini kwa wafanyakazi wote ambao wanatoka nchini ikiwa ni pamoja na kuboresha mishahara yao lakini vile vile na kuwapa vivutio. Wizara yangu kama nilivyokuwa nikisema, tayari inajitahidi kuweza kuwapa motisha ili waweze kubaki hapa lakini vile vile kuweza kuwaambia watu wetu waweze kuwa na uzalendo wa kubaki na kutumika hapa nchini.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na mikakati mizuri aliyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, hapo awali tuliwahi kuzungumzia suala hili hili, tukasema kwa sababu India ni nchi moja ambayo tunapeleka

wagonjwa wetu kwa wingi, yalitokea mapendekezo kwamba awekwe *Medical Attaché* yaani Daktari ambaye atakuwa anashughulikia kuhakiki matibabu yanayopelekwa kule hasa ukizingatia kuwa kulikuwa na baadhi ya wagonjwa tulipofika kule walibainika mwishoni wana Kwashakoo na magonjwa ambayo ukweli hawastahili kwenda kule. Kimsingi lilikubalika ndani ya nyumba hii, lakini sijui kama liliwahi kufanyiwa kazi na kama halijafanyiwa kazi ni kwa nini ili tuweze kuona na sisi Wabunge tutachangia vipi ili aweze kupatikana *Medical Attaché*. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ilitolewa rai kwamba kuwepo na *Medical Attaché* na sasa hivi Wizara yetu ilikuwa inafanya mpango wa kumpeleka kule ili aweze kuwepo kule na kuweza ku-*screen* wale wagonjwa wanaokwenda pale ambao kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba wengine wameonekana kwamba pengine hawana stahiki. Lakini vile vile tumekuwa tukisisitiza kwamba kabla hata hajafika kule India kuwepo na utaratibu mzuri zaidi wa kuweza kuwa-*screen* hapa hapa kwa sababu kuwapeleka kule kumwachia huyo *Medical Attaché* ina maana ni kumpa kazi wakati Madaktari na kamati zote zinakaa hapa kuweza kum-*screen* kabla hata hajapatiwa ile nafasi ya kwenda India.

SPIKA: Ooh, kwa upendeleo maalum, Mheshimiwa Malecela swali la nyongeza!

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali la nyongeza. Je, Wizara inayo habari kwamba *KCMC* wanafanya upasuaji wa moyo na mpaka mwaka jana walikuwa wamepasua watu 48 *successfully* na kama *facilities* hizo ziko *KCMC*, kwa nini Serikali isisaidie kujiimarisha ili badala ya kupeleka wagonjwa India ikapeleka *KCMC*?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, Wizara inayo taarifa kwamba *KCMC* wanafanya operesheni ya moyo. *KCMC* inaendeshwa kwa pesa za Serikali, kwa hiyo mipango yote inayoendeshwa pale kwa kiasi kikubwa ni pesa za Serikali. Vile vile tunaimarisha hicho kitengo na tunatambua na kuwashukuru kwa kazi wanayofanya. Lakini ieleweke kwamba operesheni zinazofanywa pale ni za msimu, hawana wataalam wa kutosha. Wana uhusiano na taasisi ya nje ambao wanakuja wanakaa kwa muda, wanafanya operesheni halafu wanaondoka. Tunachojaribu kufanya hapa ni kuwa na kitu cha kudumu na tutakapokuwa na Taasisi yetu pale Muhimbili ni kwamba wataalamu watakuwepo wakati wote na tutazidi kutafuta wengine na kuwasomesha ili kuimarisha kituo chetu.

Na. 9

Wagonjwa Waliofanyiwa Upasuaji Kimakosa

MHE. HASSAN C. KIGWALILO (K.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA) aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo mwezi Novemba, 2007 imeripotiwa kuwa katika Hospitali ya Mifupa ya *MOI* walifanya *operation* ambazo zilileta utata miongoni mwa Watanzania:-

(a) Je, ni utaratibu upi na vigezo gani vilivyosababisha kutokea kasoro hiyo mbaya ya tiba?

(b) Je, Serikali ina mpango wowote wa kulipa fidia kwa waathirika?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mnamo mwezi Novemba 2007, upasuaji tata ulifanyika katika hospitali ya *MOI* na baada ya kufanya uchunguzi wa kitaalam kupitia kamati mbili zilizoundwa, Waziri alitoa taarifa kwa Watanzania wote kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kutoa taarifa kwamba taaluma ya upasuaji kama zilivyo taaluma nyingine za afya zina taratibu za utendaji kazi za kufuata; taratibu hizi zinaitwa *Standard Operating Procedures*. *Operation* tata zilizofanyika *MOI* zilitokana na kutofuata taratibu hizi pamoja na kuaminiana baina ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya tukio hilo, ziliundwa Tume kwa ajili ya kushughulikia suala hili na kutoa mapendekezo Serikalini. Kutokana na ripoti ya Tume, Wizara ilitoa maagizo kwa Bodi ya *MOI* yakiwemo mabadiliko katika mfumo wa uongozi wa Idara na pia kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa *Standard Operating Procedures* zinafuatwa ili kusitokee tena mkanganyiko kama uliotokea awali. Aidha, watumishi 11 wa taaluma za Udaktari na Uuguzi wamepelekwa mbele ya Mabaraza ya Kitaaluma kujibu tuhuma zinazowakabili.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya kutokea upasuaji tata, Serikali ilichukua jukumu la kumpeleka mhusika nchini India kwa matibabu ambapo Serikali iligharimia matibabu, gharama za usafiri kwa ndugu na wasindikizaji na pia fedha za kujikimu. Suala la fidia ni la kisheria hivyo iwapo mgonjwa hakuridhika na huduma aliyopewa, ana haki ya kufuata mkondo wa sheria za nchi zilizopo ili aweze kupata haki yake.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pia naona jibu lake lina utata.

(a) Kwa kuwa tunazungumzia *Standard Operating Procedures* hazikufuatwa, ni nini hicho? Waziri mwenyewe aliwaambia wananchi, kwa nini hakikutajwa kwa kuwa hapa kuna mtu amepoteza maisha na pia kuna mtu mpaka hivi sasa anaendelea kupata matatizo, ni binadamu huyu!

(b) Je, huyu mgonjwa anayeendelea kupata matatizo au anaumwa, yuko wapi na anaendeleaje?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nimesema *Standard Operating Procedures* ina maana ni ule mtiririko unaoanza kuanzia mgonjwa anapoingia hospitalini mpaka anapotoka hospitalini. Anapofika pale, kwanza anapokelewa, anaonana na Daktari mpaka iamuliwe kwamba *diagnosis* yake ni ipi na afanyiwe operesheni gani na mpaka inapotokea kwamba operesheni inafanyika mpaka anapopona na kupewa ruhusa. Kwa maana hiyo, ndiyo nikasema kwamba, mambo yaliyotokea pale ni mengi, lakini katika haya ni kwamba kulikuwa kuna ukiukwaji wa kutokufuata taratibu, ndiyo maana hiyo operesheni ikawa tata kwamba kuna mkanganyiko uliotokea pale kwa kutokufuata hizi *procedures*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, mgonjwa huyu Didas alikuwa amepelekwa India, lakini mgonjwa huyu sasa hivi amesharudi yuko pale Muhimbili, anaendelea na matibabu, anaendelea kufanya mazoezi ili aweze kutembea vizuri, aweze kuongea vizuri na aweze kurudi nyumbani na kujiunga na familia yake.

Na. 10

**Faida ya Kubinafsishwa Mashamba
ya NAFCO ya Kapungu na Mbarali**

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. CYNTHIA H. NGOYE)
aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Serikali ilibinafsisha mashamba ya iliyokuwa *NAFCO* huko Kapungu na Mbarali na kuwakabidhi wawekezaji binafsi:-

(a) Je, ni mabadiliko gani yamefanyika tangu mwekezaji huyo akabidhiwe mashamba hayo na ni kwa kiasi gani ametekeleza masharti aliyopewa wakati anakabidhiwa?

(b) Je, ni wakulima wadogo wadogo wangapi wanaozunguka mashamba hayo wamefaidika tangu mwekezaji huyo aanze kazi?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili, naomba kujiunga na wenzangu katika kutoa salamu zangu za rambirambi kutokana na kifo cha Mheshimiwa Losurutia, Mbunge wa Kiteto. Namuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za rambirambi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), naomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mashamba ya Mbarali na Kapungu yalibinafsishwa kwa makampuni mawili tofauti. Mashamba haya yalitangazwa kuuzwa mwezi Agosti, 2004. Shamba la mpunga Mbarali lilibinafsishwa kwa *Highlands Estate Co. Ltd* kwa shilingi bilioni 3.5 na Kapungu kwa *Export Trading Co. Ltd* kwa shilingi bilioni 2.311. Shamba la Kapungu lilikabidhiwa kwa mwekezaji tarehe 13 Septemba, 2006 na shamba la Mbarali tarehe 14 Septemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu wawekezaji hawa wakabidhiwe mashamba hayo, mabadiliko yafuatayo yamefanyika kulingana na masharti waliyopewa wakati wanakabidhiwa:-

Kwanza, shamba la Mbarali, mwekezaji kwenye shamba la Mbarali amekwishalipa shilingi bilioni 2 kati ya shilingi bilioni 3.5 alizotakiwa kulipa. Aidha, kwenye shamba hili, mwekezaji ametumia jumla ya shilingi bilioni 2.72 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na kununua vifaa mbalimbali. Kwa shamba la Kapungu, mwekezaji alikwishalipa shilingi bilioni mbili na laki tatu ambayo ndiyo bei iliyokubalika. Aidha, mwekezaji Kapungu amenunua matrekta mapya 14, mitambo miwili ya kuzalisha umeme na pembejeo mbalimbali za kilimo ambapo ametumia jumla ya shilingi bilioni 1.2. Vile vile kwenye mashamba yote mawili, mifereji ya maji imesafishwa na hivyo kufanya mtiririko wa maji ya kumwagilia mashamba kuwa mzuri. Aidha, umeme, simu na maji vimerejeshwa. Mashamba na ukarabati wa mitambo, barabara na nyumba umefanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa shamba la Mbarali, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2007, vikundi vya wakulima wadogo wadogo 884 vilikuwa vimekodishiwa jumla ya hekta 2500. Aidha, wananchi wanaozunguka shamba, wamefaidika kupata maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo. Vile vile ajira 100 za kudumu na 200 za muda zimepatikana. Pia mwekezaji amechangia katika kukarabati Shule ya Msingi Mbarali na kujenga madarasa mawili na ofisi za Walimu. Jumla ya shilingi milioni 8 zimetumika.

Mheshimiwa Spika, kwa shamba la Kapungu, 2006/2007 jumla ya hekta 576 zilikodishwa kwa vikundi 39 vya wakulima wadogo wadogo. Aidha, mwaka 2007/2008, jumla ya hekta 786 zimekodishwa kwa vikundi 56 vya wakulima hadi kufika Desemba 2007. Zaidi ya hekta 174 zinatarajiwa kukodishwa hadi kufikia Julai, 2008.

MHE. ESTHERINA J. KILASI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa lengo la Serikali katika kubinafsisha mashamba haya ilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa kilimo cha mpunga na hatimaye kuondoa tatizo la chakula na kwa kuwa mwekezaji wa Kapungu mpaka sasa nafikiri hajaamua nini cha kufanya na

eneo la hekta 3000, ni hekta 700 tu ambalo zimekodishwa lakini eneo kubwa limekuwa likibaki bila kulimwa.

Je, Serikali haioni katika ule mkataba ambao walikubaliana kwenye *sale agreement* kwamba aongeze asilimia ya kuwakodisha wakulima kwa mpango wa *out growers* kusudi walime mpunga na wamuuzie yeye kwa mkataba, haujatekelezwa? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kabla ya kubinafsishwa mashamba haya hasa hili shamba la Kapungu, wakulima wadogo wadogo ambao ndiyo lilikuwa lengo lao la kuanzisha lile shamba kwa ajili ya *small holders*, walikuwa wanatumia muundombinu mmoja wa maji kwa maana ya *intake* kwa ajili ya kumwagilia mashamba yao lakini baada ya kuuza shamba hili, huyu aliyenunua amekabidhiwa pamoja na muundombinu huo kitu ambacho kimekuwa ni kero kwa wakulima wadogo wadogo kwa sababu maji wanayopata wakati wa msimu wa kulima ni mpaka maamuzi ya huyu mnunuzi aamue ni lini wakati wa kuwapa maji.

Je, Serikali sasa ina mpango gani ili kutimiza lile lengo la awali la kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ili watengenezewe muundombinu wa maji unaojitegemea kuwawezesha hawa wakulima waendeleo kulima na kuboresha upatikanaji wa chakula? (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, makubaliano tuliyofanya kati ya Serikali na huyu mwekezaji ni kukuza kilimo cha mpunga baada ya kuwa amefanya uwekezaji na uwekezaji unaendelea vizuri na makubaliano hayo yalikuwa kwa muda wa miaka mitano. Kwa hiyo, tunampa muda ili kuhakikisha kwamba makubaliano yaliyoko katika ule mkataba yanatekelezwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuweka mfereji ili kuwawezesha wakulima wadogo waweze kupata maji, hii ni sehemu ya makubaliano. Serikali tutasimamia kuhakikisha kwamba makubaliano hayo yanatekelezwa ili wakulima wadogo waweze kufaidi na waweze kukua na kuendelea pamoja na mkulima huyu mkubwa aliyeuziwa shamba hili. (*Makofi*)

Na. 11

Taarifa ya Ndagalu Kupatiwa Umeme wa Gridi

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa ya Ndagalu Wilayani Magu ni maarufu kwa kilimo cha pamba, mahindi, mpunga, ufugaji na kuna idadi kubwa sana ya wananchi na taasisi nyingi za umma; je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Tarafa hiyo umeme wa gridi kuanzia

vijiji vya Nh'haya, Kabila, Shishani hadi mahala ambapo kinapakana na Wilaya ya Bariadi ili iwe chachu ya kuwaletea wananchi maendeleo ya haraka?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuvipatia umeme vijiji vya Tarafa ya Ndagalu, inabidi ijengwe laini ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 kutokea Magu Mjini. Umbali kati ya vijiji ambavyo vitahusika na mradi huo ni kilomita 50 kama ifuatavyo:- Magu Mjini hadi Nh'haya km 17.5, Nh'haya hadi Kabila k.m. 11.5, Kabila hadi Shishani k.m. 13 na Shishani hadi Mahala k.m. 8.

Mheshimiwa Spika, kazi ya awali ya kupeleka umeme Mahaha kutoka Magu imekwishafanyika ambapo gharama ya kujenga laini ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Magu Mjini hadi Mahala pamoja na ununuzi na ufungaji wa transfoma na ujenzi wa laini ndogo zimeainishwa kufikia shilingi 3,700,000,000. Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (*Rural Energy Agency*) inaendelea na juhudi za kutafuta fedha ndani na nje ya nchi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Aidha, chini ya Mradi wa *Electricity "V"* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo Afrika (*ADB*), vijiji kadhaa Wilayani Magu vitapatiwa umeme. Vijiji hivyo ni Nyamatembe, Shigala, Shigala West, Ihayabuyaga, Mahangala, Nyangili North, Nyangili South, Nassa Genary, Malili, Ngunga, Ngasamo, Ngasamo Genary, Mwanangi, Mwanangi South, Mwaniga, Badugu, Busami, Busami School, Nyamikoma, Mkula na Lamadi.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza napenda kushukuru kwa niaba ya wananchi wa Magu kwa Serikali kukipanga Kijiji cha Ihayabuyaga kuwa katika vijiji ambavyo vitapatiwa umeme mwaka huu. Pili napenda niipongeze sana Serikali kwa kusikia kilio changu cha muda mrefu kwa niaba ya wananchi wa Ndagalu, cha Tarafa hiyo kupatiwa umeme ikizingatiwa kwamba imezingirwa na mto Simiwi pande zote na ikizingatiwa pia ni tarafa yenye watu wengi na taasisi nyingi na inazalisha mazao mengi na kwamba kuna wawekezaji walitaka kwenda kuwekeza vinu vya kukamulia pamba na kukamua mafuta.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwapa matumaini wananchi wa tarafa hiyo kwamba ifikapo Disemba 2010 watakuwa wamepatiwa umeme ili waanze kufurahi?

SPIKA: Na wewe pia ufurahi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Festus Limbu kama ifuatavyo:-

Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kufanya juhudi kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2010 wananchi wengi zaidi wa Tanzania wakiwemo wa Jimbo la Magu watakuwa wamenufaika na huduma ya umeme. Lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuipongeza Serikali kwa juhudi ambazo inazifanya. Changamoto iliyopo mbele yetu Mheshimiwa Spika ni kuomba tu sekta au Wizara hii ipatiwe kipaumbele ili tupate fedha nyingi zaidi za kuwafikishia huduma wananchi kwa wingi zaidi, naamini kwamba katika bajeti inayokuja Waheshimiwa Wabunge watalifikiria jambo hili.

Na. 12.

Wilaya ya Tunduru Kupatiwa Umeme wa Kutosha

MHE. MTUTURA A. MTUTURA aliuliza:-

Kwa kuwa miradi ya umeme ya Kanda ya Kusini ya Kampuni za ARTUMAS na SONGAS haitafika Tunduru kwa vile Wilaya hiyo kiutawala iko Mkoa wa Ruvuma; na kwa kuwa mradi mkubwa wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa Mkoani Ruvuma utaishia Wilaya ya Namtumbo bila kufika Tunduru ambayo ipo Mikoa ya Kusini kijiografia; na kwa kuwa Mji wa Tunduru upo katikati ya mradi wa barabara itokayo Mtwara hadi Mbamba Bay:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kuipatia umeme Wilaya ya Tunduru inayojiandaa kupokea mabadiliko makubwa kiuchumi?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kufufua mradi wa kuzalisha umeme katika maporomoko ya Sunda yaliyoko Mto Ruvuma ili kuipatia Wilaya ya Tunduru umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu sawali la Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Kampuni ya Ushauri ya *DECON* ya Ujerumani ilifanya upembuzi yakinifu wa kuipatia Wilaya ya Tunduru umeme wa uhakika. Matokeo ya Upembuzi huo yalionyesha kuwa Wilaya ya Tunduru inaweza kupata umeme unaozalishwa na nguvu ya maji kutoka katika maporomoko ya Sunda. Maporomoko hayo yako katika Mto Ruvuma takriban kilomita 82 kutoka Tunduru mjini. Upembuzi yakinifu uliofanyika miaka ya nyuma ulionyesha kwamba utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme katika maporomoko ya Sunda utagharimu Dola za Marekani milioni 16 kwa gharama za mwaka 2005. Aidha, matokeo ya upembuzi yakinifu huo yalionyesha kuwa ili mradi ukidhi mahitaji ya Tunduru kwa kipindi kirefu, inabidi ifungwe mitambo ya mafuta Tunduru ili kusaidiana na kituo cha Sunda.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Tunduru, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (*Rural Energy Agency*) Wizara inaendelea na juhudi za kutafuta fedha ndani na nje ya nchi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kuwapatia wananchi wa Tunduru umeme wa uhakika. Tunawaomba wananchi wa Tunduru wawe na subira wakati wanaendelea kutumia umeme unaozalishwa na mitambo ya mafuta iliyopo kwa sasa. Pamoja na juhudi hizo, tathmini itafanyika kuona uwezekano wa kupeleka Tunduru umeme wa gesi asilia unaozalishwa na Kampuni ya *ARTUMAS* Mtwara.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza katika maelezo yangu ya utangulizi, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi wa umeme wa maji wa Sunda. Namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Tunduru wavumilie wakati Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza azma ya kuwapatia umeme wa uhakika.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo yametolewa ambayo hayaleti matumaini ya karibu ya wananchi wa Tunduru nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa itachukua muda mrefu sana umeme wa *ARTUMAS* kufika Tunduru kwa vile hata Masasi haujafika; na kwa kuwa mgawo wa umeme kwa Mji wa Tunduru umekuwa ukiendelea mwaka hadi mwaka kwa kipindi cha mwaka mzima; je, Serikali ina mpango gani wa haraka na wa muda mfupi kuhakikisha kwamba Tunduru inapata umeme wa uhakika na wa kutosha?

(b) Kwa kuwa wananchi wa Tunduru wamekuwa wakiishi na huyu mtu anayelitwa subira kwa muda mrefu; je, Serikali iko tayari kumhamisha huyu subira Wilaya ya Tunduru na kumwelekeza Wilaya zingine hasa zile ambazo ziko mbele kimaendeleo ili na sisi Tunduru tuweze kusonga mbele? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba niseme tu kwa niaba ya Serikali kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia wananchi wa Tunduru umeme wa uhakika, lakini pia nimwombe Mheshimiwa Mbunge aungane na juhudi za Serikali kuwapa matumaini wananchi kwamba jitihada za makusudi zinaendelea.

Tusingependa kutoa kauli za kuwakatisha tamaa wananchi kwa sababu nchi hii ni yetu wote na tunafahamu uwezo wetu kwa rasilimali fedha ambazo zinawezesha kutoa huduma, mahitaji ni makubwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Tunduru kwamba Serikali inatambua kilio hiki na ndiyo maana hata Wizara

yetu imekuwa ikifanya ziara sehemu mbalimbali kuhakikisha kwamba inajionea hali halisi ya kero ambazo zinawakabili wananchi ikiwemo kupitia eneo la Tunduru ambapo Wizara yetu kupitia Wizara ya Madini ilifika kujionea hali halisi ya umeme katika Wilaya ya Tunduru. Kwa hiyo, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea.

Mipango iliyopo sasa hivi ni kuzidi kuimarisha mashine zilizopo. Kuna mitambo miwili ambayo inazalisha umeme kwa kutumia mafuta ya dizeli, na tunaendelea na juhudi kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwahudumia wananchi wa Tunduru kadri ambavyo tunaweza kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

Lakini pia Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge tukubaliane kwamba tunakosa neno mbadala la kutumia badala ya kusema neno subira kwa sababu tunaamini ni neno la kiungwana zaidi la kuwapa matumaini wananchi. Tusingependa kutumia maneno ambayo yanawakatisha tamaa wananchi lakini ukweli unabaki palepale kuwa sisi tunaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa wananchi wengi zaidi wananufaika ama wanapata huduma ambayo wanaitarajia kwa sababu tunaamini kwamba umeme pia ni nyenzo muhimu sana katika maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge tuzidi kushirikiana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 13

Nyumba za Askari wa Magereza na Polisi

MHE. MWANNE I. MCHEMBA aliuliza:-

Kwa kuwa nyumba nyingi wanazoishi askari polisi na askari magereza ni chakavu sana na nyingi zimejengwa wakati wa ukoloni:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzibomoa na kujenga nyumba mpya?
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kushirikisha vyombo vya fedha kama vile *NSSF, PPF* n.k. katika kutatua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mbunge wa Viti Maalumu, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mbunge wa Viti Maalumu, kuwa nyumba nyingi wanazoishi askari polisi na askari wa magereza ni chakavu sana kwa sababu nyingi zilijengwa zamani hasa wakati wa ukoloni. Pia zilizopo hazitoshelezi mahitaji ukilinganisha na idadi ya askari waliopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa askari kuwa na makazi bora. Ili kuhakikisha kuwa askari wanaishi katika mazingira mazuri, Serikali kupitia bajeti ya Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati nyumba zilizochakaa na kujenga nyumba mpya kwa kutumia fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kubomoa nyumba zilizochakaa na kujenga mpya na za kisasa unafanyika Serikali inapokuwa na fedha za kutosheleza kujenga nyumba mpya. Kwa mfano hivi sasa Jeshi la Polisi limebomoa nyumba zilizochakaa eneo la *Kilwa Road*, jijini Dar es salaam, muda si mrefu mradi wa kujenga nyumba mpya za askari utaanza. Kwa upande wa Jeshi la Magereza mradi wa kubomoa nyumba zilizochakaa na kujenga mpya umeanzia Gereza la Iringa mwaka 2006/007 ambapo jengo lenye ghorofa nne linaendelea kujengwa. Ghorofa hilo litakuwa na uwezo wa kuishi familia 16 za askari na kila familia itakuwa na vyumba viwili vya kulala, sebule, jiko na bafu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kushirikisha vyombo vya fedha kama vile *NSSF* na *PPF* katika kutatua tatizo la nyumba za askari. Kama ushahidi wa kutambua hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana katika Ibara ya 29(f)(ii), (iii) na (iv) ya Hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 katika ukurasa wa 38 alilitaarifu Bunge hili kuwa *NSSF* imetenga fedha kwa ajili ya majeshi kama ifuatavyo:-

- (i) Ujenzi wa nyumba za Jeshi la Wananachi shilingi bilioni 21.544.
- (ii) Ujenzi wa nyumba za Jeshi la Polisi shilingi bilioni 10.0.
- (iii) Ujenzi wa za Jeshi la Magereza shilingi bilioni 34.

Mheshimiwa Spika, utumiaji wa mafungu hayo yaliyotengwa utaanza mara baada ya mdhamana wa Hazina (*Treasury Guarantee*) utakapotolewa.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ambayo yamejitosheleza na nimeridhika nayo, naomba niongeze kidogo. Kwa kuwa bajeti ya 2007/2008 kama alivyokiri mwenyewe, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, alikuwa ametenga fedha hizo; na kwa kuwa sasa hivi tuko kwenye mchakato wa 2008/2009, bajeti hiyo bado haijatekelezeka; na kwa kuwa Kanuni ya fedha inasema ifikapo bajeti nyingine ile pesa ambayo haijapitishwa wala kuridhiwa huwa inakuwa ime-*corrupt*; je, ni kigugumizi gani kilichoifanya Wizara ya Fedha isitoe *guarantee* ya hizo bilioni 44 mpaka sasa tunapoingia kwenye mchakato mwingine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningependa tutofautishe ukarabati na ujenzi wa majengo ambao uliwekwa ndani ya bajeti ambao unatekelezwa na pesa zile ambazo zimeombwa kupitia mfuko wa *NSSF*, *PSPF* na *PPF*. Kama nilivyoainisha kwenye jibu langu la msingi, kwenye bajeti yetu ya 2006/07 imeelezwa kwamba tutaendeleza ukamilishwaji na ukarabati wa nyumba za askari katika magereza na vituo vifuatavyo:-

Gereza la Mpwapwa, Muleba, Arusha, Chuo cha Ukonga, Chuo cha Kiwira, gereza la Keko, Morogoro, mahabusu Iringa, kambi ya Kimbiji na Luanda Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kama alivyouliza katika swali lake na kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, Serikali inaona umuhimu wa kutumia mifuko ya *PSPF*, *NSSF* katika kujaribu kuboresha makazi ya askari. Na kama nilivyoeleza pale ambapo *treasury guarantee* itatolewa, hizi bilioni 34 ambazo zimetengwa kwa ajili ya majengo ya askari magereza zitatolewa na zitatumika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita. Yale maswali mawili yaliyosalia ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi tutayapa kipaumbele katika vikao vinavyofuata. Matangazo! Nianze na wageni. Wageni wetu Bungeni leo hii ni kama ifuatavyo:-

Wapo wageni wa Mheshimiwa Mbunge Getrude Rwakatare kama ifuatavyo: Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Morogoro. Kwa taarifa tu ingawa Mbunge anaitwa Rwakatare lakini anatoka Morogoro. Wengine ni Mwenyekiti na Katibu wa UWT, Wilaya ya Kilombero anakotoka Mheshimiwa Mbunge. Waliobaki ni wachungaji, wazee wa kanisa na baadhi ya washirika wa Kanisa la Mikocheni B *Assemblies of God* ambako anahudumu Mchungaji Rwakatare. (*Makofi*)

Karibuni sana, tunashukuru kwa kuja kumwunga mkono Mheshimiwa Mbunge Rwakatare na ahsanteni pia kwa kazi njema mnayoifanya kwa jamii. Nafurahi sasa kumkaribisha mgeni mwingine, naye ni mke wa Mheshimiwa Castor Ligalama na wana-CCM kutoka jimbo la Kilombero. (*Makofi*)

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ambao ni Mchungaji John Masha na Mchungaji Christopher Milimo, sijui wametoka Kilindi au wapi! Yupu mgeni wa Mheshimiwa Mpesya, ni kijana wake, Stanslaus Lambert maarufu kama Nyerere kutoka shule ya Sekondari Mbeya. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nafurahi kuwaarifu kwamba mwenzetu Mheshimiwa Fatma Athuman ambaye alikuwa amelazwa pale *MOI* sasa hali yake ni ahueni na ametoka hospitali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na mkutano wa Kamati ya Huduma za Jamii leo hii saa tano asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema tumebakiza shughuli moja tu kwa sababu Muswada ulioiva ni mmoja tu na leo nadhani ndiyo kutakuwa na jitihada za kukamilisha Miswada mingine. Kwa kawaida hatuweki Muswada mmoja wakati ambapo muda bado upo kwa sababu unaweza ukaisha halafu tena tukaahirisha Bunge, kwa kuogopa usumbufu huo nimeona kwamba tutasikiliza kauli ya Waziri baada ya hapo itanibidi niliahirishe Bunge.

KAULI ZA MAWAZIRI

Taarifa ya Hatua zilizochukuliwa na Serikali katika Akaunti ya EPA

WAZIRI WA FEDHA: Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kwa masikitiko kutoa pole kwa familia ya marehemu, Mheshimiwa Benedict K. Lusurutia aliyekuwa Mbunge wa Kiteto aliyefariki dunia mwezi Disemba, 2007, tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahala pema peponi, Amen.

Pili, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Getrude Rwakatare, kwa kuwa Mbunge Viti Maalumu, nasema pongezi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Mkutano huu wa Bunge kwa mwaka huu, napenda kuwatakieni heri ya mwaka mpya wa 2008.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba wakati wa Mkutano wa Bunge wa kujadili bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, Serikali iliahidi kuwasilisha Bungeni taarifa na hatua zilizochukuliwa na Serikali mara ya baada ya ukaguzi wa hesabu za mwaka 2005/06 za Akaunti ya Malipo ya Madeni ya Nje kukamilika. Aidha Serikali ilikwisha agiza toka tarehe 4 Disemba, 2006 kuwa ukaguzi huo ufanyike baada ya kupata taarifa kutoka kwa Mkaguzi wa Hesabu za Nje za Benki Kuu, *Delloit and Touche*.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano wa Bunge la Bajeti mwaka 2007/08 unaendelea, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walihoji kuhusu tuhuma mbalimbali dhidi ya Benki Kuu ya Tanzania. Serikali kwa nyakati tofauti ilitoa maelezo ndani ya Bunge kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha kama ifuatavyo:-

“Tarehe 22/06/07 wakati wa majumuisho ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/08, Waziri wa Fedha alizungumzia taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu kuhusu taarifa zilizokuwa zimesambazwa katika mtandao wa intaneti zilizomhusu aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kuwa, “Serikali inazo taarifa hizo zinazotoa shutuma mbalimbali dhidi ya Gavana wa Benki Kuu na baadhi ya wafanyabiashara hapa nchini. Hata hivyo, Serikali haiwezi kutoa

tamko lolote kwa kuwa chanzo cha habari hizo hakijathibitishwa, na mara nyingi habari za intaneti hazina uhakika kama ni za kweli au za uwongo. Aidha, ina vyombo vyake vya kufuatilia.”

“Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitaka pia maelezo kuhusu tuhuma za ubadhirifu wa fedha katika Akaunti ya Biashara ya Nje katika Benki Kuu. Ningependa kutoa maelezo kwamba Serikali ilimwagiza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kusimamia uchunguzi huu. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekwishaalika Kampuni za kimataifa za ukaguzi wa hesabu zilete zabuni zao kwa kazi hiyo. Zoezi hilo linategemewa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu, nawashauri Waheshimiwa Wabunge wavute subira ili tupate uhakika baada ya ukaguzi huu kufanywa kwenye mahesabu yale ya benki.”

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 2 Julai, 2007 wakati wa majumuisho ya Bajeti ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa maelezo kama ifuatavyo:-

“Tumechukizwa na kushtushwa na taarifa kwamba kuna fedha zimepotea ndani ya Benki Kuu, kwa hiyo, baada ya kuchukizwa kwa jambo lenyewe tumemwagiza *Controller and Auditor General*, tunamwamini ni mtu shupavu ashirikiane na *Audit* za Kimataifa wakague Benki wajue imekuwaje jambo hili kama ni la kweli; je, ni kweli? Nani anahusika? Ni akina nani na tuchukue hatua gani ili jambo hili lisije likatokea tena kama kweli imetokea? Kwa hiyo, Serikali tumechukua hatua kabla ya kuja hapa, hivyo nawasihi wenzangu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba jamani jambo hili halihitaji Kamati Teule ya Bunge, baada ya taarifa hiyo kupatikana tunachukua hatua zinazopasa na Bunge hili litaarifiwa.”

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Serikali iliahidi kutoa taarifa Bungeni baada ya ripoti ya ukaguzi kukamilika, naomba sasa kuwasilisha rasmi taarifa na hatua zilizochukuliwa na Serikali kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Mwaka 2005/06 katika Akaunti ya Malipo ya Madeni ya Nje, *EPA* katika Benki Kuu uliofanywa na kampuni ya ukaguzi ya nje, *Ernest and Young* na ripoti yake kukabidhiwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambaye baada ya kuridhika nayo aliiwasilisha ripoti husika kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 7 Januari, 2008.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa taarifa na hatua zilizochukuliwa na Serikali ningependa nitoe historia fupi ya *EPA*. Katika miaka ya 1970 mpaka 1990 nchi yetu ilikumbwa na uhaba mkubwa wa fedha za kigeni ambapo Benki Kuu ya Tanzania ilipewa jukumu la kusimamia matumizi ya fedha za kigeni kwa niaba ya Serikali. Benki Kuu ndiyo ilikuwa na mamlaka ya kupanga ni nani wa kugawiwa fedha za kigeni na kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ili kuwahudumia wafanyabiashara, mashirika na makampuni yanayoagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, akaunti maalumu ilifunguliwa katika iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara, ambayo ilijulikana kwa jina la *External Payment Arreas* au Akaunti ya Malipo ya Madeni ya Nje, kwa tafsiri ya Kiswahili.

Waagizaji wa bidhaa au huduma kutoka nje waliwajibika kulipa kwenye akaunti hiyo fedha ya Tanzania yenye thamani sawa na fedha za kigeni zinazotakiwa kulipia bidhaa au huduma hiyo huko nje. Baada ya waagizaji wa ndani kufanya hivyo kutegemeana na upatikanaji wa fedha za kigeni, wauzaji au watoa huduma za nje walilipwa na Benki ya Biashara baada ya kupata kibali cha Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Juni, 1985 Serikali iliamua kuwa shughuli za Akaunti hiyo zihamishiwe Benki Kuu ya Tanzania kutoka Benki ya Taifa ya Biashara na zinaendelea kuwepo hapo hadi sasa. Aidha, katika Benki Kuu kiliundwa kitengo maalum cha kusimamia na kuendesha shughuli za Akaunti hii kitiwacho *Debt Management Unit* chini ya Kurugenzi za Sera za Uchumi (*Directorate of Economic Policy*). Kwa sababu ya tatizo la upungufu wa fedha za kigeni kuendelea malimbikizo ya madeni hayo yalizidi kukua mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, hadi kufikia mwaka 1999 deni hilo lilifikia dola za Kimarekani milioni 623. Kati ya fedha hizo dola milioni 325 ndilo deni la msingi na dola milioni 298 ni riba, baadaye likaongezeka kufikia dola za Kimarekani milioni 677.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kulipa malimbikizo ya madeni hayo zilifanywa wakati wote kadri fedha za kigeni zilivyopatikana. Kwa nia ya kutafuta ufumbuzi wa haraka wa tatizo hilo na kupunguza mzigo wa madeni, Serikali ilianza kutafuta njia mbadala mbalimbali. Mwaka 1994 Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, ilianzisha mpango wa kununua madeni (*Debt Buy Scheme*) yaani wadai waliombwa wakubali kulipwa sehemu tu ya madeni wanayodai na baadhi ya wadai walikubaliana na mpango huu. Taarifa za mwaka 2004 zinaonyesha kuwa madeni ya thamani ya dola milioni 228 zililipwa chini ya mpango huu.

Aidha, Serikali ilifanya juhudi za kupata msamaha wa madeni. Taarifa ya mwaka 2005 inaonyesha kuwa madeni yenye thamani ya dola milioni 228 milioni yalilipwa chini ya mpango huu. Aidha, Serikali ilifanya juhudi za kupata msamaha wa madeni hayo kutoka nchi wanachama wa *Paris Club*. Serikali iliomba kuwa pamoja na kusamehe madeni ya Kiserikali toka nchi zao, wasaidie pia kusamehe madeni ya makampuni yao. Yapo madeni yamelipwa na makampuni ya bima baada ya kampuni yaliyouza bidhaa na huduma Tanzania kushindwa kulipwa.

Madeni ya dola milioni 216 yalikusika chini ya michakato hii. Hivyo deni la dola milioni 444 lilipungua katika jumla ya dola milioni 677 na kubakia dola milioni 233 mwaka 2004. Yalikuwepo mawazo ya baadhi ya watu walioshauri kuwa deni hilo lisilipwe au tulikatae. Walikuwepo pia waliokubali madeni hayo yafutwe na wengine waliagiza fedha zao zilipwe *NGO*. Lakini baadhi ya wadai waliendelea kudai na wengine hata kuishitaki Serikali mahakamani. Hivyo Benki Kuu iliendelea kulipa kadri wadai walipojitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa malipo ya madeni ya *EPA* kanuni zinaruhusu mdai kuamua deni lake kulipa yeye mwenyewe au kwa mtu au kampuni nyingine. Kanuni zinamtaka mdai kutoa hati iliyothibitika kisheria na yeye kuidhinisha

malipo hayo yafanywe (*notarised deed of assignment*). Pia yapo masharti ya kutimizwa na kampuni au mtu aliyeidhinishwa kulipwa deni hilo. Utaratibu huu umetumika katika kufanya malipo kadhaa ya madeni katika akaunti ya *EPA*.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutofuata utaratibu wa kulipa madeni ya *EPA* lilijitokeza katika ukaguzi wa hesabu za Benki Kuu kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Katika ukaguzi uliofanyika wiki ya mwisho ya mwezi Agosti, 2006, iligundulika kuwa waliolipwa hawakustahili kwa kuwa nyaraka zilikuwa batili, hali hii ilileta kutoelewana kati ya Benki Kuu na Mkaguzi wa Nje wa Mahesabu aliyegundua tatizo hili. Baadaye mkaguzi huyo alisitishwa na Benki Kuu kuendelea na kazi.

Serikali baada ya kupata barua kutoka kwa Mkaguzi, tarehe 4 Desemba, 2006 ilimwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*Controller and Auditor General*) kuhakikisha kuwa ukaguzi wa akaunti yote unafanyika kwa kina. Aidha, ilimwagiza atafute kampuni ya Kimataifa ya ukaguzi ifanye kazi hiyo kwa niaba yake. Maelekezo haya pia yalitolewa kwa vyombo vya habari.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ndiye kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu Mkaguzi wa Hesabu za Benki Kuu. Hata hivyo, kwa mazingira hayo maalumu Serikali ilimtaka *Controller and Auditor General* atafute mkaguzi mwingine wa nje.

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alifanya hivyo na mchakato wa kutafuta kampuni hiyo ulichukua miezi mitano, kuanzia Januari hadi Mei, 2007 ndipo ikapatikana kampuni ya *Ernest and Young*.

Mheshimiwa Spika, wakaguzi wa *Ernest and Young* walianza kazi hiyo Septemba, 2007 na kukamilisha Desemba, 2007. Wakaguzi hawa wamefanya kazi nzuri iliyothibitisha kiwango cha juu cha ujuzi wao. Serikali inawapongeza. Tunatambua kuwa walipata matatizo mengi kuhusu madeni haya ya miaka 27 na zaidi iliyopita. Kumbukumbu zilihamishiwa kutoka *NBC* kwenda *BoT*. Hata huko *NBC* shughuli zilikuwa zinafanywa katika matawi mbalimbali nchini. Tena miaka hiyo hapakuwa na kompyuta. Hivyo kumbukumbu zote ziliwekwa kwenye majalada. Hata hivyo ukaguzi wa hesabu hizo ulikamilika kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2005/2006 uliochunguzwa katika mwaka 2005, yalifanywa malipo ya jumla ya shilingi 133,015,186,220.74 kwa makampuni 22 ya hapa nchini. Makampuni hayo ni: *Bancom International Limited of Tanzania, VB and Sources Company Limited of Tanzania, Bina Resorts Limited of Tanzania, Venance Hotel Limited of Tanzania, Njake Hotel and Tours Limited, Malta Mining Company Limited of Tanzania, Man Planners and Consultancy, Bora Hotels and Apartments Limited, BV Holdings Limited, Ndovu Soaps Limited, Nevika Tobacco Tanzania Limited of Tanzania, Changanyikeni Residential Complex Limited, Kagoda Agriculture Limited, G and T International Limited, Excellent Services Limited, Mibale Farm, Liquidity Sea Services Limited, Clayton Marketing Limited, MS Rashitasi Tanzania Limited, Malegesi Law Chambers Advocates, Kiloloma and Brother, Cannel Limited.*

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 90,359,078,804 zililipwa kwa makampuni 13 ambayo yalitumia kumbukumbu, nyaraka na hati zilizo batili na za kughushi, hivyo makampuni hayo hayakustahili kulipwa chochote. Makampuni hayo ni *Bancom International Limited of Tanzania, VB and Sources Company Limited of Tanzania, Bina Resort Limited of Tanzania, Venance Hotel of Tanzania, Njake Hotel and Tours Limited, Malta and Mining Company of Tanzania, Man Planners and Consultancy, Bora Hotel and Apartment Limited, BV Holdings Limited, Ndovu Soaps Limited, Nevika Tobacco Tanzania Limited of Tanzania, Changanyikeni Residential Complex Limited, Kagoda Agriculture Limited.*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi umeendelea kubaini kuwa makampuni 9 ambayo yalilipwa jumla ya shilingi 42,656,107,417, hayakuwa na nyaraka za kuonyesha stahili ya malipo na hivyo kuwafanya wakaguzi washindwe kuhakiki uhalali wa malipo hayo. Makampuni hayo ni *G and T International Limited, Excellent Services Limited, Mibale Farm, Liquidity Services Limited, Clayton Marketing Limited, MS Rashitashi Tanzania Limited, Malegesi Law Chambers Advocates, Kiloloma and Brothers na Cannel Limited.*

Wakati huo huo makampuni 2 yaani *Rashitashi Tanzania Limited* na *G and T International Limited* kumbukumbu zake za usajili katika Daftari la Msajili wa Makampuni hazikuweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kama mlivyosikia kupitia taarifa iliyotolewa na Serikali, Mheshimiwa Rais, baada ya kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ya Mkaguzi wa Nje (*The Ernest and Young*) alisikitishwa na kukasirishwa na ukiukwaji wa makusudi wa sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza matumizi ya fedha za umma na alichukua hatua zifuatazo:-

- (1) Alitengua uteuzi wa aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu, Dr. Daudi Balali.
- (2) Alimteua Profesa Beno Ndulu ambaye wakati huo alikuwa Naibu Gavana kuwa Gavana mpya wa Benki Kuu na pia alimteua Dr. Enosi Bukuku aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu kuwa Naibu Gavana masuala ya Sera na Fedha.
- (3) Aliagiza Bodi ya Benki Kuu ikutane mara moja kujadili taarifa ya ukaguzi na kuchukua taarifa zipasavyo za kinidhamu dhidi ya maofisa wa benki walio chini ya mamlaka yake waliohusika na kusababisha hasara hii kwa taifa.
- (4) Aliteua Kamati Maalumu inayojumuisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na *Inspector General* wa Polisi kuchunguza na kuchukua hatua za kisheria zipasazo kwa makampuni na watu waliohusika na uhalifu huu.
- (5) Rais amewataka watumie ipasavyo mamlaka na madaraka waliyonayo kwa mujibu wa sheria. Aidha, Kamati hii imepewa muda wa miezi 6 kukamilisha kazi hii.

Amemwagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuwa kiongozi wa kazi hii na kuwataka wahakikishe kuwa fedha zilizolipwa isivyo halali zinarudishwa. (*Makofi*)

(6) Rais, amemtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kushirikiana na kuwasaidia watendaji wakuu wa vyombo vya dola katika kufanikisha jukumu hilo. Aidha, watu wengine wenye taarifa za ziada wameombwa pia wazitoe kwa Kamati. Shughuli za ulipaji madeni katika akaunti ya *EPA* zisimamishwe mara moja mpaka taratibu za uhakiki na utaratibu mpya utakapotengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Fedha nayo imechukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, Waziri wa Fedha, alifanya uteuzi wa wajumbe wa Bodi mpya ya Benki Kuu kwa mujibu wa Kifungu cha 9 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Na. 4 ya Mwaka 2006 ambapo wajumbe 6 hutumikia kwa mujibu wa nyadhifa zao za kiofisi (*ex-official*) na wajumbe 4 huteuliwa na Waziri wa Fedha.

Bodi hii ilizinduliwa rasmi tarehe 21 Januari, 2008. Katika uzinduzi huo Waziri wa Fedha aliagiza Bodi hiyo mpya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya maafisa wote wa Benki Kuu walio chini ya mamlaka ya nidhamu ya benki ambao walihusika na tatizo hili. Aidha, alitoa changamoto kwa Bodi kuhakikisha inarejesha imani ya wananchi kwa chombo hiki chenye dhamana kubwa ya kusimamia hazina ya taifa na mwelekeo wa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Wizara ya Fedha ni kama ifuatavyo: Kwanza, Mamlaka ya Mapato Tanzania imepewa maagizo ya kufanya uchunguzi wa kina kubaini mienendo ya ulipaji kodi wa makampuni yote yaliyohusika na endapo itabainika kuwepo ukwepaji wa kodi, hatua za kisheria zitachukuliwa. (*Makofi*)

Pili, Benki Kuu ya Tanzania imeelekezwa kufanya uchunguzi wa kina na kuwasilisha taarifa Serikalini kuhusu hatua zilizochukuliwa kwa mabanki ya biashara yaliyohusika na kupokea fedha kutoka makampuni husika endapo sheria, taratibu na kanuni kuhusu udhibiti wa fedha haramu zilizingatiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kwa dhati kabisa itahakikisha kila mtu au taasisi iliyohusika na tuhuma zilizotajwa katika ripoti ya wakaguzi inachukuliwa hatua zinazostahili kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi.

Tatu, hoja kuhusu kufanyika kwa uchunguzi wa ubadhirifu katika akaunti ya *EPA* ilitokana na agizo la Serikali kufanya ukaguzi maalumu wa matumizi ya akaunti hiyo tangu tarehe 4 Desemba, 2006.

Nne, Serikali iliahidi kuwasilisha Bungeni taarifa na hatua ilizochukua baada ya kukamilika kwa ukaguzi jambo ambalo inatekeleza leo hii kupitia tamko hili.

Tano, Serikali inawaomba wananchi kuwa na subira wakati Kamati iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais, ikikamilisha uchunguzi utakaothibitisha kisheria tuhuma zilizobainishwa kwenye taarifa ya ukaguzi ili wahusika waweze kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Sita, kama ambavyo Mheshimiwa Rais alivyoagiza, wananchi wanaomba kutoa ushirikiano wa dhati kwa Kamati kwa kutoa taarifa zitakazoweza Kamati kukamilisha majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa John Cheyo, chini ya Kanuni ipi?

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kanuni mpya hatuna hapa ni vigumu kunukuu Kanuni hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Naikubali hoja yako endelea! (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa taarifa hii ni muhimu sana na nyeti na kwa kuwa hatua nzuri zimekwishachukuliwa na Mheshimiwa Rais na taarifa nzuri imetolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ametuomba wananchi tushirikiane, naomba kwanza mwongozo wa Spika, kuhusu taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kama hiyo taarifa itafika kwenye Meza yako ili iweze ikajadiliwa kama vile taarifa zingine za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali?

La pili, kama kabla ya hiyo taarifa haijafika kwako kama Mheshimiwa Spika, utatoa ruhusa kwa Bunge hili kuweza kujadili taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri, ili Waheshimiwa Wabunge na wenyewe waweze wakatoa busara zao juu ya jambo hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako! (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka nadhani linaungana na hilo hilo.

MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na niliyokuwa nimeomba kuhusu mwongozo wako. Kutokana na ukweli kwamba sasa hivi hatuna Kanuni mpya na kutokana na unyeti wa jambo hili na ahadi ya Serikali kwamba italetta taarifa hiyo ya mkaguzi kuhusu fedha za EPA na kwamba ingeleta kwenye Bunge hili; na kwa kuwa kilichowasilishwa na Waziri ama ni *summary* tu au *extract* ya kile ambacho naamini kuwa kitakuwepo kwenye taarifa hiyo, sasa naomba mwongozo wako, kama itakubalika uielekeze Serikali watulettee taarifa

kamili ya mkaguzi na siyo *extract* kama ilivyofanyika ili Bunge hili ipate fursa ya kuijadili kwa kina.

Na kwa kuwa wakati wa kujadili Hotuba ya Waziri Mkuu niliomba kuundwa au nilipendekeza kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge na kwa maana hiyo naomba mwongozo wako iwapo kuwepo kwa taarifa hii kunaweza kuathiri kwa kuletwa hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ili muhimili wa Bunge nao uweze kutimiza nafasi yake ya kuwawakilisha wananchi kujua undani wa yaliyotokea kwenye Benki Kuu. Nilikuwa naomba hili lifanyike na kama haliwezekani utupe mwongozo ili tujadili taarifa iliyoletwa hapa, hicho kipengele kidogo kilicholetwa ili kutenda haki ukweli uweze kubainika. Naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge aliyoyasema Mheshimiwa John Cheyo na ameongezea Mheshimiwa Christopher Ole – Sendeka, yote yalikuwa katika mchakato wa mashauriano baina ya ofisi yangu na Serikali. Kwa hiyo, katika muda ambao ni muafaka ndani ya wiki hii tutawapeni taarifa ya jinsi ya kulishughulikia jambo hili. Niseme tu kwamba msisahau nilikwisha kubali hoja ya Mheshimiwa Lucy Mayenga katika Mkutano wa Tisa, ambaye baada ya taarifa ya mahesabu ya mwaka 2005/2006 ya Benki Kuu kuwasilishwa Mezani, alisimama chini ya Kanuni husika kuomba kwamba taarifa ipagiwe muda ijadiliwe. (*Makofi*)

Hata kama Serikali haitataka ombi hilo la Mheshimiwa Lucy Mayenga bado liko hai na kwa hiyo nitakuwa sina kipingamizi chochote. Kwa kweli ni wajibu wangu kuhakikisha kwamba tutaanzia hapo kwa Mheshimiwa Lucy Mayenga ila kama itakuja taarifa nyingine ndefu, kwa zama hizi za uwazi na ukweli na nadhani Serikali imesikia, bila shaka tutafikia mahali pazuri. Katibu kuna shughuli zinaendelea? (*Makofi*)

KATIBU WA BUNGE - BW. DAMIAN S.L. FOKA: Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo tumefikia mwisho wa shughuli zilizokuwa zimepangwa kwa leo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama alivyotangaza shughuli zilizotangazwa kwa Kikao cha leo zimekamilika. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.20 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi siku ya
Jumatano, Tarehe 30 Januari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*